

18

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG**

**SIMU NA :027-2530022  
2530042**



**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),  
S.L.P. 2,  
KATESH-HANANG,  
MANYARA.**

**NUKUSHI NA  
:027/2530022  
:027/2530042**

**30/08/2021**

**TANGAZO LA ZABUNI YA UTOAJI WA HUDUMA YA USAFI WA  
MAZINGIRA (UZOAJI TAKA NGUMU) KATIKA MJI WA KATESH  
LIMERUDIWA – LIMEONGEZWA MUDA  
ZABUNI NA. LGA/059/2021/2022/NC/03**

1. Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' katika kuboresha usafi wa mji wa Katesh inakusudia kupata mzabuni wa kufanya kazi ya kuzoa Taka ngumu kwa kutumia wakala au watu binafsi au makampuni kuzoa taka kwenye maeneo yote ya mji wa Katesh.
2. Halmashauri ya Wilaya ya Hanang inawatangazia wananchi wote, watu binafsi na Makampuni kuomba Zabuni ya utoaji wa huduma ya usafi wa mazingira (uzoaji wa taka ngumu) katika maeneo yote ya Mamlaka ya mji mdogo wa Katesh .
3. Usafi huo utafanyika maeneo yafuatayo; - KATESH, GANANA, JORODOM NA DUMBETA - Kukusanya takataka (taka ngumu na laini) katika masoko, kwenye maeneo ya biashara na maeneo ya makazi na kupeleka dampo.

<b>Namba ya Zabuni</b>	<b>Jina la zabuni</b>	<b>Wanaostahili</b>
<b>Zabuni Na. LGA/059/2021/2022/NC/ 03</b>	<b>Zabuni ya kutoa Huduma ya usafi wa Mazingira (uzoaji wa taka ngumu) katika maeneo yote ya mji wa Katesh</b>	<b>Makampuni, Taa sisi, Vikundi na watu binafsi.</b>

## MASHARTI YA ZABUNI YA UKUSANYAJI WA ADA ZA USAFI NA MAZINGIRA.

Barua za maombi ziambatanishwe na maelezo kamili na vivuli vya nyaraka zilizothibitishwa.

1. Mwombaji wa Zabuni anatakiwa kulipa ada ya maombi ya Zabuni kiasi cha Tshs 50,000/= benki ya NMB baada ya kupewa Bill na Mhasibu wa Mapato Halmashauri ambayo haitarudishwa
2. Mwombaji lazima awe amesajiliwa kisheria.
3. Mwombaji atakayeshinda Zabuni atalazimika kutumia mashine ya Kielektroniki "Point of Sale"(POS) na ataweka fedha zote katika Akaunti ya Halmashauri. Wakala atarudishiwa "Commission" isiyozidi **asilimia (95%)** Mwombaji ataje asilimia atakayorejeshewa kwa chanzo hiki.
4. Mwombaji aambatanishe maelezo ya kazi alizowahi kuzifanya.
5. Mwombaji asiwe Mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang (A Public Officer) au Mheshimiwa Diwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang.
6. Mwombaji wa Zabuni lazima aambatanishe kiapo cha dhamana ya Zabuni (bid security declaration). Format yake iko katika kabrasha la Zabuni.
7. Mwombaji asiwe na deni lolote katika Halmashauri ya Hanang'.
8. Mwombaji anatakiwa awe na vitendea kazi vya usafi kama nguvu kazi watu, magari(lorry), overcoat , gloves, refractor n.k
9. Mwombaji atakayefanikiwa kuwa Mzabuni atakusanya Ada kulingana na viwango vilivyowekwa na Halmashauri pamoja na Sheria Ndogo za Halmashauri (By-Laws).
10. Kama kutatokea kutoeleweka au kutoelewana katika utekelezaji wa sharti lolote la Mkataba utakaofungwa kati ya Halmashauri na mshindi wa Zabuni pande zote mbili zitakaa na kutatua tatizo kwa njia ya majadiliano. Ikiwa majadiliano yatashindwa kuleta muafaka suala hilo litapelekwa kwa msuluhishi ambaye ni Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tawi la Katesh na ikiwa usuluhishi utashindikana shauri la suala hilo litapelekwa Mahakamani.



11. Mwisho wa kutuma maombi ya Zabuni ni siku ya Jumatatu tarehe 08/09/2021 saa 5:00 asubuhi kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'.

Barua zote za maombi ziandikwe kwa anuani ifuatayo:

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG,  
S.L.P 2,  
KATESH – HANANG**

12. Maombi ya zabuni ambayo hayataletwana kupokelewa na kusomwa siku ya ufunguzi hayatakubalika.

*Jenifa C. Omolo*

**Jenifa C. Omolo**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG.**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA  
HANANG**

**NAKALA:**

1. Ofisi ya Katibu Tawala. –Wilaya ya Hanang'  
S.L.P 10  
KATESH/HANANG'
2. Watendaji wa Kata - Wajulisheni wananchi katika  
Kata zenu.
3. Mbao za Matangazo